

COASTWEEK inafuraha kutangaza kwamba Said A. Burhan sasa ndiye Mhariri mpya wa Kurasa ya Swahili. Bw. Said Burhan amekuwa mwandishi kwa muda mrefu na mwalimu maarufu sana mjini Mombasa. Amewahi kuwa mshindi wa wandishi wenye mashindano ya B.B.C. na mwalimu wa Swahili katika shule kadha Pwani.

MOMBASA MAGHARIBI YAMTAFUTA MBUNGE WAKE

KUNGANA NA malalamisho niliyoyapata kutoka kwa wanachi wa sehemu ya Mombasa West ni kwamba, hawajui wamba Mjumbe wao wanaweza kumuona wapi. Tabu nyingi wazo hawana wakumueleza ila tu Makaunsila na wana KANU wama hiyo.

Tumejaribu kufanya Harambee zetu sa skuli lakini yeye alungaliki kabisa na tunasikitika kusema kwamba maeneo engine ya Mombasa ambayo M.P.'s, Kaunsila, KANU Chairmen wadhirikiana harambee zao zinaendelea vizuri.

Kilingana na mwito wa Rais wetu Mheshimiwa Daniel Arap oi baada ya Bunge kufungwa wabunge warudi maeneo yao ontu nipango ya maendeleo yake inaendelea vizuri na itakuwa a sisi kuomba msaada wa Wabunge wengine na wetu yuko Kaonekani.

Juper Walele,
Kwani, MOMBASA.

Lengo la Buibui ni Kuusitiri mwili siyo kuusaidia maasi

KINADAMU WALIANZA kuihifadhi miili yao mara tu waipobukiwa na fikra ya kuwa manyoya ya miili yao hayakutosha kuwa ni kinga ya mwili wao thamani ambao wanepewa na Mola. Na ndipo wakaanza kutengeza ngozi na huta magamba ya miti ili kupata hivadhi tosha ya miili yao. Hizo hazikuwa zamani za kuchagua nimbara hiki na kile katika maduka aula yaliyosambaa sika mabarabara shamshama.

Huta hivyo viumbe hao ambao kwa mujibu wa wataalamu wa tarehe na maumbile ya viumbe wa mwanzo elo mababu zetu, wanastahiki pongezi kwa vile kuamua wa mwili wa mwanadamu ni lazima usitiriwe. Kwa nini umbe hivyo vya myaka laki walukuki vyastahili sifa? ababu ni kwamba hivi leo baada ya ulimwengu wote arban kustarabika, kunao watu miongoni mwetu ambao engineo ati wamesoma na ambao mpaka hivi sasa wwajuzina haja ya mwanadamu kujistiri mwili wake hasa ambapo hadharani.

Tumesoma kwa wanazuoni kwamba mwili wote wa wanamke wahitajiwa usitiriwe kikamili wakati wa wanamke huyo atokapo hadharani na ikamlazimu hakuna na wanaume wasiokuwa maharimu zake. Sababu ni kwamba, mwili wa mwanamke mara moja huleta hamsoso. Lakini mapinduzi ya elimu na ustarabu wa haja mila za wagaeni, umewalazimisha wasichana wachukia buibui kama wanavyomchukia nyoka mweusi. Wengine hulivaa buibui ili tu asikaripiwe hapo kwao. Lakini hapo ti akishaitoka nyumba yao, hulipandisha juu hilo buibui ati anataka kuonesha miundi ya miguu. Wengine hulivaa kitambara cha buibui kinachoonya na hivyo hawa buibui hilo halikuleta sitara yoyote ya mwili. Halafu hawa pia mabuibui ya Saudia. Mabuibui haya, bada ya kusitiri mwili wa mwanmke, huzidi kumletea fitna. Hawa hawa wakuuliza, jawabu lao ni kwamba ati biashara ni biashara. Madhumuni hasa ya mwanamke kuvalia buibui, ni kuhakikisha kwamba mwili wake toka maguu hadi uso havionekani. Leo ni kinyume nyume, kwa maana mavazi ya buibui limefungwa ncha ya kisogo hali manywele yamefunuliwa timu timu, mtindo huu huitwa 'hunting' (Ndi).

Kwa ili kuwa banati za kiislamu zenyewe zimeshindwa kuvaliwa kivazi chao cha heshima, wameyakaribisha na kuyaiga mengine na dini zengine kulituyuri na kulivurujua kabisa. Hadi ya kufikia kuwa leo halina tena thamani. Tumeshamishwa kwamba siku hizi wasichana wa kibara, wakiwa ti ushaniwe wavulana hasa wakijomba, basi huvaa buibui! Na pia tumefahamishwa kwamba wasichana wengine hata wa nchi za jirani pia huvaa buibui wakati wanapokwenye majumba ya matata, ili ionekane wote wanaokwenda huko ni banati wa Kiislamu.

Kwanini nangonja maoni yenu kubusu rai ya kurudisha mitindo ya buibui.

Jee Waislamu, mwashindwa kuwavisha jamii zenu vazi la stara!

ZAMANI Waswahili walisema "Mwacha asili ni mtumwa". Leo tunaona dhahiri shahiri hakika ya msemo huu, kwani aghalabu ya watu sasa wametupa asli zao lijamu, hawafurukuti, wasemayo mabwana zao huwa ndiyo.

Tunayaona haya katika usemi kwa kuchanganyisha maneno ya kigeni katika lugha ya Kiswahili na katika kivazi, kwa kutupwa vazi la heshima na stara na kuvaa kivazi kisichoelekea na Sharia, na katika mengi mengineyo ambayo kwayo twachelea makama na adhabu ya Mwenyezi Mungu.

Leo tutataja lile ambalo ni muhimu zaidi na ambalo likiachwa litaleta hatari zaidi. Hapa tukumbushane mmoja katika misemo ya Kiswahili isemayo: "Akipewa shubiri huchukuwa pima", tutaona kuwa Mwenyezi Mungu amewatukuza wanawake na kuifanya miili yao kuwa na yenye thamani kubwa na kwa hivyo akawaamrisha wajistiri kiwiliwili chote isipokuwa Vitanga Vya Mikono na Uso peke yake, viungo ambavyo kwa desturi lazima vitumike. Akasema:

(Ewe Mtume! Waambie wake zako na binti zako na wanawake wa Kiislamu wajiteremshie uzuri ushungi wao ili wajulikane kuwa ni watu wa heshima wasiudhiwe, na Mwenyezi Mungu wa kusamehe na mwingi wa kurehemu. Qurani: 33:59)

Akasema tena:

Na waambie Waislamu wanaume wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao, hili ni takaso kwao; bila shaka Mwenyezi Mungu ana habari za yote wayafanyayo. Na waambie waislamu wanawake wainamisha macho yao na walinde tupu zao, wala wasidhihirishe viungo vyao isipokuwa vinavyodhihirika navyo ni uso na viganja vya mikono na waangushe shungi zao mpaka vifuani mwao, na wasionyeshe mapambo yao ila kwa waume zao, baba zao baba za waume zao)wakwe zao), watoto wao, watoto wa waume zao (watoto wao wa kambo), kaka zao, wana wake kaka zao wana wa dada zao, wanawake wenziwao au wale iliyowamiliki mikono yao (watumwa zao) au wafuasi wao wasokuwa na matamanio au watoto ambao hawajajua mambo yaliyohusu uke. Wale wasipige miguu yao ili yalijulikana wanayoyaficha katika mapambo yao, na tubieni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waislamu ili mpate kufaulu. Quran: 24:30-31.

KIVAZI halisi cha Mwanamke wa Kiislamu.

Lakini wapi! Inahuzunisha kweli! wanawake wameshukuwa pima na zaldi Ya pima wanaona kila kiingiacho mjini halali ijapokuwa cha feliyaani kitendo kibaya hawana heshima hata na baba zao wanakaa wakibeheneka na kubahashuka uchi mabarabarani na hadharani hawajali makatazo ya Mola wao.

Ufisadi umeenea na ufasiki umetapakaa na wazee na wenye kuhusika kimya wamezibwa midomo bali na masikio na macho pia yote yanayopita hawayaoni. Hasara ilioje jamani kuacha ndugu zetu waasi hadharani wapate laana ya Manani kesho Akhera na hapa duniani.

Basi inataka tutanabahi na itutoke kasumba ya kutamalakiwa na fikira na mila za kigeni, tushika-mane na mila ya dini yetu ya Kiislamu iliyomtukuza na kumuenzi na kumthamini mwanamke kwa kumvesha kivazi cha staha na stara.

Mwenyezi Mungu amesema katika Qurani yake tukufu:

Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtumewe wakatapo shauri, kuwa na hiari katika shauri lao, na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtumewe, hakika amepotea upotevu wa dhahiri (33:36).

Hapa inataka ifahamike kuwa kwenda kinyume na Sharia ya Mwenyezi Mungu ni kosa na hatia ambayo ina madhara makubwa. Na kwa kuwa Mwenyezi Mungu keshaamrisha wanawake kujistiri basi hebu tujulishane kivazi cha Sharia kikoje:

Kivazi kiwe cha stara na cha heshima kinyume na kile wavaacho wanawake wachafu.

Kiwe kimefunika mwili mzima isipokuwa uso na viganja vya mikono.

Kisionye kwa wepesi wake na kudhihirisha vya ndani.

Kiwe bwagabwaga kisibane mpaka kikadhihirisha maungo.

Kisiwe ni kivazi cha kiume au chenye kushabihiana nacho kama suruali n.k.

Kisiwe kama kivazi cha wanawake wa kikafiri kwani Muislamu anatakiwa atafautiane nao kwa kila kitu.

Kisiwe kivazi cha fakhari cha kudhihirisha kiburi.

Pamoja na haya, mwanamke hatakiwi kutia manukato na kujipaka marangi ya kila aina hadharani. Hayo hufanyiwa mume tu nyumbani. Halikadhalika haruhusiwi kulegeza sauti na kwenda mwendo wa kukatisha kwani haya yote husababisha kuzindua matamanio na kuleta uasherati na uzinzi.

MOLA SAMAHANI

Basi na tukome na kuleta fisadi mijini, la si hivyo basi Mola ni sultani na hapana mwenye hasira zaidi kuliko yeye Manani. Basi tuche tufani ambayo ikija haioni huzoa wote Motoni.

Ewe Mola wetu samahani. Na kwa Mfume wako amani. Nasi tuzidishie Imani. Ya rabbal-alamini.

SALIM ELHAJ

COASTWEEK JISHINDIE

Miavuli maridadi katika shindano jipya la kujaza

SWAHILI CROSSWORD NO. 123



JINA .....

SANDUKU LA POSTA .....

.....

KWENDA KULIA:

1. Jina la zamani la mji wa Mombasa.
5. Mtoto wa ng'ombe.
7. Wewe
8. Kinyume cha P.M.
10. Ukavu, aradhi isiyo na maji.
12. Kidonda kikubwa.
13. United Kingdom.
14. Kitambulisho cha mtu.
15. Ua changa.
16. Safisha, toa uchafu.
17. Tibu, fanyia dawa mtu.

KWENDA CHINI:

1. Chombo cha muziki.
2. Ngoma kubwa.
3. Sema.
4. Weka juu ya jiko.
6. Zuia vita.
9. Teketea.
11. Panga gutu.
14. Mahali pa taka.
15. Tosha, basi.

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 122

Walter Kingi Chengo, Sanduku la Posta 274, MALINDI.

Simeon Tawa, c/o Jimba F.P. School, P.O. Rabai, RURUMA

Master Kavulunze D. Mulwa c/o D. M. Kinyunge, Sanduku la Posta 46550, NAIROBI.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 122 —

KWENDA KULIA:

1. TEMBO, 6. TUNZA, 7. RINDA, 8. MKATE, 10. ETI, 12. WA, 13. IANZE, 15. IMBA, 17. UBAO, 19. FURAHI.

KWENDA CHINI:

1. TARISHI, 2. MENDE, 3. OTAMIA, 4. ONJA, 5. WAMEA, 9. TWEKA, 11. TIARA, 14. NDUI, 16. MTU, 18. OA.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindi watatu kila baada ya wiki mbili watapata miavuli maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK LIMITED, Mombasa.

Jawabu za Fumbo hili lipelekwe kwa Mhariri, COASTWEEK, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Jumatano tarehe 12.8.81 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.